



**COUNTY ASSEMBLY OF MOMBASA
THE HANSARD**

Tuesday, 27th February, 2024
Third Assembly – Third Session
FIFTH SITTING

*[The County Assembly met at 11:05a.m. at the County Assembly Buildings]
[The Speaker (Honourable Aharub Ebrahim Khatri) in the Chair]*

PRAYERS

The Speaker (Hon. Khatri): Honourable Members, you may be seated. Yes Clerk, next Order please?

[Consultations]

MOTION

APPOINTMENT OF MEMBERS TO THE COUNTY ASSEMBLY BUSINESS COMMITTEE

Yes, Honourable Athman Rama Mwamwiri, Leader of Majority party please move the Motion?

The Leader of Majority (Hon. Mwamwiri): Thank you Mr. Speaker Sir. Mr. Speaker, I beg to move the following Motion,

THAT pursuant to the provisions of Standing Order 151 (1) (d), this Assembly approves the appointment of the following Members, nominated by the County Assembly parties to be Members of the County Assembly Business Committee in addition to those specified in Standing Order 151, 1(a), (b) and (c) :-

1. Hon. Prischillah Mumba
2. Hon. Abdirahman Hussein
3. Hon. Maryam Baimu
4. Hon. Frankline Makanga
5. Hon. Mwinyi Mtoto
6. Hon. Hawa Abdirahman
7. Hon. Ibrahim Omondi
8. Hon. Kibwana Swaleh
9. Hon. Milka Ngare

10. Hon. Naeem Shafiq

May I beg Honourable Prischillah Mumba, the Majority Chief Whip to second the Motion, thank you.

Majority Chief Whip (Hon. Mumba): Thank you Mr. Speaker. I second the Motion.

The Speaker (Hon. Khatri): Honourable Members, I now propose the Motion by Honourable Athman Rama Mwamwiri on the approval to serve in the County Assembly Business Committee to be considered in the same terms as moved.

[Question proposed and agreed to]

Yes, Honourable Athman Rama Mwamwiri Leader of Majority Party please, make your contribution? The Leader of Majority.

The Leader of Majority (Hon. Mwamwiri): Thank you Mr. Speaker. Mr. Speaker as provided in the Standing Order that immediately after long recess the Assembly amongst the first business is to approve the Members of the House Business which there after shall be the answerable considered to undertake the planning and approval of business to be tabled in this House. Mr. Speaker, the membership of this Committee is very much in order the gender issue has being considered and majority of the Members served in the previous Committee and we have an introduction of new Members which is healthy succession plans that we do introduce some Members so that they can as well understand and get the experience from the senior Members. I, therefore urge the Honourable Members to approve these Members so that we can proceed with businesses as required in the service to the County, to our people. Thank, you Mr. Speaker.

The Speaker (Hon. Khatri): Yes, Honourable Fadhili Makarani?

The Deputy Speaker (Hon. Fadhili Makarani): Ahsante sana Mheshimiwa Spika kwa kunipa fursa hii ya kuweza kuongea mbele ya Bunge letu. Mimi nachukua wakati huu kupongeza Kamati teule ya Nyumba ambayo itaweza kufanya kazi na chini ya taratibu zetu za Bunge. Mheshimiwa Spika, Kitengo cha 25 na Kamati hii ina jukumu kanuni za kudumu (1)(2)(3) kwenda mbele Kamati hii ina jukumu la kuweza kutengeneza kalenda ambayo itaweza kutuweka sisi katika vikao vya Bunge hili. Mheshimiwa Spika na twaelewa ya kuwa mwezi Mtukufu wa Ramadhan uko karibu na mimi nachukua fursa hii kabla ya Mheshimiwa Spika kuomba Kamati kama itakapokuwa imeweza kupitishwa na kalenda hiyo itakuwa ni jambo la kwanza kabisa baada ya Kamati kupitishwa kuletwa katika Bunge letu ili iweze kwenda kuchapishwa kule kwa *Government Printers*. Mheshimiwa Spika, naomba Kamati iweze kuweka katika fikra zao mwezi huu Mtukufu wa Ramadhan ili iweze kutupatia wakati wa sisi kuweza kufanya ibada. Kwa hayo Mheshimiwa Spika mimi narudi kukaa lakini nawaomba Wenzangu tushirikiane pamoja tupitishwe hii Kamati ili kazi na majukumu yetu yaanze ndani ya Bunge letu. Ahsante sana.

The Speaker (Hon. Khatri): Thank you very much Honourable Fadhili Makarani, the Deputy Speaker. Yes, Honourable Mbaya please make your contribution?

Hon. Hamisi Mbaya: Ahsante sana Mheshimiwa Spika kwa kunipatia nafasi hii. Mheshimiwa Spika nimesimama kuunga mkono uteuzi wa majina ambayo yameweza kufikishwa mbele yetu kwa asilimia 90 kwa 100. Mheshimiwa Spika, nikiangalia majina ambavyo yameweza kuorodheshwa hapa Mheshimiwa ambaye ametuanzia pia ni miongoni mwa wale wakongwe; Mheshimiwa Prischillah Mumba ambaye ni miongoni mwa wale ambao tunawategemea katika Nyumba hii. Mheshimiwa Spika, vile vile nikienda kwenye nambari 9 ambayo inanipa uzito kuunga mkono uteuzi wa Kamati hii namuona Mheshimiwa ambaye ni Mheshimiwa Milka Moraa Ngare ambaye ni miongoni mwa wale ambao ni wazoe fu kwa haswa kwa mipangilio ya kuongea kwa Kiingereza tofauti na kama sisi. Mheshimiwa Spika, naona sababu ni nyingi ambazo zinasababisha tuweze kuunga mkono uteuzi wa Kamati hii kwa sababu nikiingia upande ule mwingine wale ambao ni wazee kama sisi naona mzee mwenzangu nambari 8 ambaye ni Mheshimiwa Kibwana Swaleh pia ameweza kuorodheshwa katika Kamati hii ambaye pia ni mzoefu katika Jumba hili. Mheshimiwa Spika kama ni kuongea, nitaongea tu sana na itakuwa vile vile sio vyema la msingi na la muhimu niweze kutambulika kwamba nimeunga mkono Kamati hii kwa uteuzi huu. Ahsante sana Mheshimiwa Spika.

[Applause]

The Speaker (Hon. Khatri): Thank you very much. Yes, Honourable Nyota, please make your contribution?

Hon. Hamisi Nyota: Thank you so much Mr. Speaker. I stand to support the Motion Honourable Speaker; first of all, I like the blending of the Members in this Committee and this is good practice that we have these settings where Members are swapped to different Committees so that they can learn more. So, Honourable Speaker I also support that there is gender equality in this list so I think it is good practice and I stand to support this important Motion. Thank you, Honourable Speaker.

The Speaker (Hon. Khatri): Thank you Honourable Nyota. Yes, Honourable Mwaka Mwalundonda?

Hon. Mwaka Bakari: Ahsante. Ahsante sana Mheshimiwa Spika; mwanzo nimshukuru Mwenyezi Mungu muumba ardhi na mbingu na viumbe vyote vilivyo ulimwenguni kwa kuweza kumaliza likizo salama salmin na tumeregea hapa Bungeni tukiwa sote tuko salama salmin. Kwa hilo namshukuru Mwenyezi Mungu, mimi mwenyewe pia namshukuru Mwenyezi Mungu najisikia niko na nguvu sana kipindi hichi ambacho nimerudi mpaka Mwenyekiti wangu ameniambia mbona umenenepa, nimenenepa kweli Mwenyekiti! Ahsante. Ahsante sana, napenda kuunga mkono Kamati hii ambayo kwamba imeteuliwa sasa hivi, hususan sana sana kama mimi mwenye ambaye ni kiongozi mteule na naona wenzangu hapa wamepata nafasi watatu na hilo nasema shukran sana Bwana. Spika. Pili vile vile naona pia hao kina mama tumepata nafasi nne hapa katika Kamati hilo nashukuru sana kwa kuweza kulitia maanani kuweza kupata nafasi hii, naomba Mwenyezi Mungu awajaalie hichi kipindi ambacho kiko sasa cha House Business kiwe ni kipindi ambacho kitaleta manufaa na kuweza kutuletea biashara nzuri ndani ya Bunge hili na pia vile vile kutujali viongozi wenzenu ambao hatuko katika hii Kamati. Ahsante sana Mheshimiwa Spika.

The Speaker (Hon. Khatri): Thank you very much. Yes, Honourable Silvester Kai?

Hon. Kai: Thank you, Mr. Speaker and for my Senior Honourable Prischilla Mumba, I just want to say sorry, I believe you could be the one speaking before me but I guess the Speaker he was not able to see that you were standing. I want to take this opportunity to join my fellow Members to support this new Motion. Having in mind that we have been in to a long recess and therefore we are having a backlog of businesses so the idea of adding the three Members so that we Fasttrack the business we have in this Assembly goes so well with me but again we cannot underrate the seniority of the Members that have been added in this Committee. A good example Honourable Kibwana Senior and again Honourable Prischilla Mumba but again I do believe we are going to enjoy the eloquence of English, from our very own from Kisauni Honourable Milka Ngare and therefore, I fully support this Motion and I wish you all the best as you embark on your new roles. Thank you very much Mr. Speaker.

The Speaker (Hon. Khatri): Thank you Honourable Silvester Kai. Yes, Honourable Prischilla Mumba.

Hon. Mumba: Ahsante Mheshimiwa Spika. Nashukuru na nashukuru pia Mheshimiwa Kai kunipa heshima yangu katika Nyumba; ninashukuru Mheshimiwa Spika kunipa nafasi hii na zaidi ninataka kushukuru Waheshimiwa wote kwa afya na uzima na kuweza kukutana tena salama. Mimi nimekuwa Mwanachama wa hii Kamati, sikuwa ati ni mgeni ni kuwa ninaendelea na kitu ningeomba Waheshimiwa wenzangu katika hii Kamati wakati tulipokuwa tukifanya hii kazi tumeona uzito mmoja wa kuwa saa nyengine misaada kwetu inakuwa changamoto kwa sababu Waheshimiwa, sio ati uone wenye wameandikwa hapa peke yake ndio wanaweza kuhudhuria hivi vikao ni muhimu ukiwa na hoja yako yoyote, uweze kuhudhuria hivi vikao. Hapa ndio kunaletwa mambo yote ya ndani ya Bunge, yanapitia kwenye Kamati hii. Kwa hivyo hata kama huna nafasi, unaweza kuchukua Mwanachama mmoja katika hii Kamati na aweze kuleta hoja yako ikiwa umeshikika lakini ni muhimu sana katika hii Kamati tuweze kuitumia sote kama waheshimiwa ili tuweze kuona mafanikio yatakayo kuwa katika hili Bunge letu maana Kamati hii ikilala ama ikikosa Miswada basi kutakuwa hakuiingi jambo lolote hapa ndani ya hili Bunge. Kwa hivyo, ninawaomba Waheshimiwa wenzangu, tupitisha Kamati hii tupate kuendelea na kazi zetu ili tuweze kuendeleza Kaunti yetu na mahitaji ya watu wetu ambao walio tutuma katika Jumba hili tukufu. Ahsante Mheshimiwa Spika na Mungu atubariki.

The Speaker (Hon. Khatri): Thank you very much Honourable Prischillah. Yes, Honourable Nyache?

Hon. Nyache: Ahsante sana Mheshimiwa Spika na mimi kuweza kuniona. Nimesimama kuunga hoja hii, iliyokuja na Kiongozi wa Wengi, Mheshimiwa Mwamwiri. Kusema ukweli hoja hii ni muhimu sana na vile tumeona hii Kamati hapa imechaguliwa hii ni Kamati ya nguvu, Mheshimiwa Spika. Kwanza nikiangalia hio nambari ya kwanza, kiongozi mwenyewe ambaye ni Mheshimiwa Prischillah Mumba ametuonyesha mfano kwamba hapa tayari anaanza kazi kwa sababu ametuelezea kwamba hii Kamati imechaguliwa si ya kwamba ni yao pekee yao. Na sisi pia tumechaguliwa mashinani tunaweza kuingia katika ile Kamati nasi tukaleta hoja zetu. Kwa hivyo nampongeza sana mama Prischillah Mumba ametuonyesha mfano ya kwamba anaiweza hii kazi. Na hata hawa wengine pia nawapongeza kwa kuweza kuteuliwa katika Kamati hii ilioko tu nawaombea kila la heri waweze kufanya vizuri katika Kamati hii ili tuweze kufanya kazi zetu za serikali ya Kaunti kama vile kawaida kwa sababu tumetoka kwenye likizo kwa kweli tumekaa kwa muda mrefu sana. Sasa najua watachangamkia hii kazi. Ahsante sana Mheshimiwa Spika, nasimama kuunga mkono.

The Speaker (Hon. Khatri): Thank you, very much Honourable Leila. Yes, Honourable Maimuna Salim. Please make your contributions.

Hon. Maimuna Salim: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa fursa hii. mwanzo namshukuru Mwenyezi Mungu kutujalia kuwa hai na kuweza kuona siku hii ya leo. Mimi nimesimama kuiunga mkono hoja hii kwa sababu tulikuwa kwa likizo ndefu kwa hiyo ni vizuri vile Kamati ya *Selection* imeweza kukaa ikaweza kutuletea Kamati ya kuweza kuleta hoja katika Bunge na sisi kama Waheshimiwa kama alivyotangulia Mheshimiwa Mwenza ya kwamba tuna haki ikiwa tuna jambo lolote tuweze kuingia hatujafungiwa nje. Lakini sote hatuwezi kuwa viongozi wa kuzungumza na sauti moja, kwa hiyo ni viongozi ambao tumechagua wenzetu waweze kutuwakilisha katika Kamati hiyo, na tushirikiane na wenzetu tuweze kuhakikisha ya kwamba Bunge letu imeleta Miswada mizuri mizuri na tuweze kufanya kazi pamoja. Huno ni mwanzo mwingine, kwa hiyo naomba ushirikiano wenu na ikiwa Mungu ametujalia, tuweze kukaa na kufanya kazi pamoja kama Wabunge tulio chaguliwa na wananchi. Mheshimiwa Spika, mimi ninaunga mkono kwa sababu nina imani na wenye wako pale ni watu wenye wako na uzoefu wa kazi wanajua wanafanya nini na hata ambaye hajui anafanya nini ataweza kuelekezwa. Kwa hivyo mimi nimesimama kama Mheshimiwa Maimuna kuweza kuunga mkono na naahidi ya kwamba tuko pamoja na tutafanya kazi pamoja kama Waheshimiwa wa Mombasa. Ahsante sana Mheshimiwa Spika.

Hon. Speaker (Hon. Khatri): Thank you very much Honourable Maimuna. Yes, Honourable Mohammed Khamis, please make your contributions.

Hon. Mohammed Khamis: Ahsante sana Mheshimiwa Spika. Mwanzo ningelipenda kutoa shukrani zangu zote kwa Bwana Allah kutuweka sisi salama na uhai na afya kukutana tena kwa siku hii ya leo. Nashukuru tena Bwana Spika kwa kunipa fursa hii. Kitu nilichosimama zaidi nimesimama kuunga mkono Kamati hii na zaidi sababu zangu ni moja au mbili, naona *gender factor* imekuwa *considered*. Pili naona MCA's wateule wako mule ndani. Tatu, naona kuna watu ambao ni wageni hawana uzoefu na Kamati kwa hivyo wamepatiwa nafasi ya wao pia kufanyia kazi kwenye moja mwa Kamati kuu za hii Nyumba. Hili ni jambo au wazo ambalo limekuwa zuri sana na linatia imani na motisha zaidi kwa wale ambao hawajapata nafasi. Kwa hivyo nimesimama kuunga mkono Kamati hii mia kwa mia. Ahsante sana.

Hon. Speaker (Hon. Khatri): Thank you very much Honorable Mohammed Khamis. Yes, Honourable Athman... Yes, Honourable Nusura, please make your contributions.

Hon. Nusura Mwinyi: Ahsante sana Mheshimiwa Spika, kwa kunipa nafasi hii. Kwanza nataka kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuweka salama wakati wa likizo ndefu ambao tulikuwa tumekaa nyumbani nafikiri sote tulirudi mashinani kujumuika na wananchi, kwenda kuona shida ambazo ziko kule na kutatua moja, mbili, tatu na pia namshukuru Mwenyezi Mungu tumerudi salama, sote tuko hapa na sote ni wazima. Mimi pia nataka kusema nimeona hapa tumewakilishwa vizuri kama kina mama, tumeona hapa Mheshimiwa Prischillah yuko hapa, Mheshimiwa Milka yuko hapa, Mheshimiwa Hawa yuko hapa na Mheshimiwa Maryam Baimu yuko hapa. Mimi pia nataka kusema ni furaha kubwa kuona kwamba tumewakilishwa ki sawa sawa kwa sababu hapakuwa na ubaguzi hapa wa kuwa labda pengine wameingia wale wote ambao walikuwa ni wa zamani ambao wana uzoefu naona Mheshimiwa Mohamed hapa amesema maneno ambayo ni ya ki sawa sawa kwamba mpaka wale wateule wako ndani.

Mpaka wale ambao hawana uzoefu wako ndani ili wale waliyozoea ambao wana ueledi zaidi wawe watakuwa wamewabeba hawa ambao wanajifundisha sasa nao pia watakuwa wanasoma kupitia kwao. Mheshimiwa Spika hii ni kazi nzuri iliyofanyika nawapa kongole wale waliofanya kazi hii; halafu pia nataka niseme nimesimama kuingia mkono. Mheshimiwa Spika nataka kusema ahsante sana kwa wale wote ambao wameshughulika na kazi hii Mwenyezi Mungu awabariki sana.

The Speaker (Hon. Khatri): Thank you very much Honourable Nusura Mwinyi. Yes, Honourable Athman Rama Mwamwiri you may reply to the Motion?

The Leader of Majority (Hon. Mwamwiri): Thank you Mr. Speaker. Mr. Speaker as I register my appreciation to all Members for contributing and most important supporting this Motion, for the purposes of record Mr. Speaker I want to make it clear that in addition to the 10 Member listed in this list as provided in the Standing Orders No.151 (a, b and c) the other Members are the Speaker who shall be the Chairperson of that Committee, the Leader of the Majority and the Leader of the Minority also are Members of that Committee. Also Mr. Speaker the responsibility to this Committee as stated in Standing Order No.151 (5) the roles of this Committee are;

- a) To prepare and if necessary, from time to time adjust the County Assembly Calendar with the approval of the County Assembly;
- b) Monitor and oversee the implementation of the County Assembly Business and programs;
- c) Implement the Standing Orders, respecting the scheduling of programs of the Business of the County Assembly and the functioning of the Committees of the County Assembly;
- d) Determine the order in which the reports of the Committee shall be debated in the County Assembly and;
- e) Also, may take decisions and direct issues and get guidelines to prioritize or postpone any business of the County Assembly acting within the concurrence of the Leader of Majority Party and the Leader of the Minority Party as the case may be.

So, for that case Mr. Speaker I think it is clear the roles of this Committee that you are not there to debate Businesses or Motions of Members but to plan at what time and when should that Business appear before the County Assembly. Thank you, Mr. Speaker and thank you to all Members.

The Speaker (Hon. Khatri): Thank you very much Honourable Members. Honourable Members, I now put the question that the Motion by Honourable Athman Rama Mwamwiri on the *Approval of Members to serve in the County Assembly Business Committee* be approved by this Honourable House in the same terms as moved.

[Question put and agreed to]
[Applause]

ADJOURNMENT

Honourable Members, this House stands adjourned until Tuesday, 27th February, 2024 at 2:30p.m.

The House rose at 11:30a.m.

DISCLAIMER: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor Page 6*